

## **AINA ZA NAJISI.**

Najisi inayotoka katika njia mbili tupu ya mbele na tupu ya nyuma zipo aina nyingi miongoni mwazo ni;

1. Mkojo na haja kubwa.
2. Wadyi ni umaji maji mweupe mzito unaotoka baada ya mkojo.
3. Madhiyi ni umaji maji unaoshikana unatoka wakati wa hisia.
4. Ama manii ni twahara, lakini inapendezwa yaoshwe yakiwa bado hayajakauka, na yapikichwe au kusuguliwa yakiwa yamekauka.
5. Mikojo au kinyesi cha mnyama ambaye nyama yake hailiwi ni najisi, lakini mkojo au kinyesi cha mnyama ambaye nyama yake inaliwa sio najisi.
6. Damu ya hedhi na damu ya nifasi(kujifungua) ni najisi.

Najisi zote hizo tulizozitaja hapo juu ni lazima zisafishwe kwa kutumia maji, na kuziondoa sehemu zilizopo kwenye nguo au mwili isipokuwa manii ya binadamu.

Ama madhiyi ikiwa yataingia kwenye nguo inatoka kwa kuyasafisha kwa kurayarashia maji tu.

## **MIONGONI WA HUKUMU ZA NAJISI.**

1. Mtu akipatwa na kitu akawa haelewi je, ni najisi au sio najisi? Sio lazima yeye kujiuliza swali hilo, itamuwajibikia yeye kuiosha hiyo sehemu, kwani asili ya kila kitu ni TWAHARA.
2. Ikiwa mtu amemaliza kusali akaangalia mwilini kwake au kwenye nguo yake kuna najisi hakuwa ni mwenye kujua tokea mwanzo, au alikuwa anajua lakini akasahau, swala yake itakuwa sahihi katika kauli sahihi ya wanavyuoni.
3. Ikiwa sehemu yenye najisi hainekani kwenye nguo na mfano wake, ni wajibu juu yake kuiosha sehemu anayodhania kuwa najisi imekuwa hapo, kwani najisi hisiyi inayoonekana ina rangi yake, ladha yake au harufu yake, ikiwa dhana yake haelewi sehemu iliyopo najisi basi ataiosha nguo yote.